# UQAB

Jarida la

**Toleo 4**
**Mei 2017 MILADI**
**Shaban 1438 AH**

**Bajeti na Mzigo wa Maisha ya Juu kwa Mtu wa Chini**

**Somali "Eneo la Vita"**

**Kupambana na Itikadi Kali**

**Namna ya Kuhesabu Pato la Taifa (GDP)**

**Nani wa Kulaumiwa?**

**Siasa ya Kivitendo ya Marekani Juu ya Urusi Na China**




# Misimamo Mikali Ni Njama Ya Kirasilimali Kuwapiga Vita Waislamu Na Uislamu Safi

hizb.or.ke HT_KENYA htkenya ht_kenya YouTube Hizb Ut-Tahrir Kenya

# Misimamo Mikali Ni Njama Ya Kirasilimali Kuwapiga Vita Waislamu Na Uislamu Safi



Umma Wakiislamu unazidi kusononeka na kukaribia kukata tamaa kutokana na dhulma na mahangaiko wanayopitia kila uchao. Dhulma hizi zikiwa zinatokana na miito kama “Vita dhidi ya Ugaidi”, “Vita Dhidi ya Misimamo Mikali” nk… ambayo imepelekea Umma wa Kiislamu kuhisi machungu yasiyostahiki hata wanyama na miti kupitia! Miito hii hutumika kuendeleza dhulma dhidi ya Umma wa Kiislamu. Ili kuweza kufahamu na kupata uhalisia wa mambo ni vyema kujiuliza ni nini maana ya miito hii. Amma nini Ugaidi tayari limejadilliwa sana. Amma Misimamo Mikali ndio linalopigiwa debe kwa sasa. Nini Misimamo Mikali? Misimamo Mikali kwa mujibu wa sayansi ya kisiasa inamaanisha msukumo unaolenga kubadilisha jamii na mabadiliko hayo yawe ni kupitia njia za mageuzi (www.vocabulary.com). Pia humaanisha kuathiri au kubadilisha msingi asili (mapenduzi) wa jambo/kitu. Kwa hivyo neno lenyewe kibinafsi halileti maana ya jambo zuri au baya, bali matumizi yake pamoja na maneno mengine ndio itakayo julisha uzuri au ubaya wa kilicholengwa. Amma kwa miaka ya karibuni neno hili limepewa istilahi mpya iliotoka kutoka vitengo vya usalama vya Marekani na Yuropa kumaanisha wenye kulenga mapinduzi ya kimsingi kwa miondoko ya kijamii ilio zoeleka kupitia misimamo itakayo pelekea fujo na umwagikaji wa damu. Wakafanya majina haya- Ugaidi na Misimamo Mikali kuwa ni sawa yakitumiwa kuchafua wale wanaolenga kuleta mabadiliko katika ulimwengu. Na kwa kuwa hakuna waliobeba mfumo wa kimaisha tofauti na unaotawala sasa wa Kirasilimali ulioharibu mazingira wa Mwanadamu kuishi, iwe ni kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiilimu nk… ila Waislamu na mfumo wao wa Uislamu wanaouamini na kuulingania usimame badala wa huu ulioko, wamebandikizwa jina kuwa ni wenye Misimamo Mikali kama walivyo bandikwa jina kuwa ni Magaidi. Haya si mageni kwani katika historia ubandikizaji wa majina ili kuhalalisha dhulma dhidi ya watu limekuwa likijirudia mara kwa mara. Kenya yajifanya kusahau historia yake pale Mabepari wa Kiengereza walipoitawala na kuwapa walowezi ardhi ilio na rutuba nzuri na kuwafurusha wenyeji wakaishi mwituni. Dhulma zilipozidi wenyeji wakasimama kimakundi makundi kutetea haki na ardhi zao, ikiwemo Mau Mau ambao ndio lilikua kundi kubwa na lenye kutishia umakinifu wa Ubepari wa Waengereza hapa Kenya. Ili kupambana na kundi hilo Serikali ya Kiengereza iliamua kutia hofu jamii hio kwa kutekeleza mauaji ya kiholela, na yalifanyika haya baada kulitangaza kundi hilo kuwa ni la Kigaidi! Bali hawakutosheka hapo, wale walioshikwa na jeshi la Kiengereza walipelekwa kwa Daktari mkuu wa akili, J.C. Carothers, ambae kuwa baada ya uchunguzi alidai ana ushahidi wa kisayansi kuwa mwamko wa Mau Mau dhidi ya Waengereza si wa kisiasa bali ni kutokana na upungufu wao wa akili! Ukitaka kumuua Mbwa mwite koko!

Hivyo twaona kuwa Misimamo Mikali ni pazia inayotumika moja kwa moja kumlenga Muislamu yeyote na popote alipo bora tu awe anapodai mabadiliko ima ni ya kibinafsi au kama jamii kupitia Uislamu wake kama mfumo kamili wa Maisha! Hii ikiwa ni jambo lakutarajiwa maanake kiasili tangu kuumbwa ulimwengu na kuwekwa binadamu na uhai ndani yake basi kuna mapambano kati ya Haki na Batili yanayoendelea mpaka Yaumul Qiyama. Lakini kwa karne hii na mwishoni mwa karne ya kabla ya hii kumeshuhudiwa mapambano mazito kati ya Uislamu kama mfumo utokao kwa Muumba dhidi ya Mfumo Batil wa Urasilimali unaotokamana na akili finyu za binadamu hususani kutoka magharibi! Mapambano haya yanaendelea kiasi kwamba Urasilimali ambao unadhaminiwa na kupigiwa debe ulimwenguni kote na Marekani na washirika wake kupitia miito ya Uhuru, Demokrasia, Soko Huru n.k; ambao kufikia sasa wameshindwa kudhibiti wimbi linalodai mageuzi ya kupitia Mfumo wa Haki wa Uislamu baada ya kuuona kuwa Urasilimali umefeli kuwasimamia wanadamu ulimwenguni kote. Kwa sababu ya mapambano haya imeipelekea Marekani na washirika wake kubuni sheria, mbinu au sera zinazolenga kusitisha au kutia kikwazo katika kasi ya wanaotaka mageuzi kupitia Uislamu kama mfumo; hivyo kukabuniwa miongoni mwa sera ni Kupambana na Ugaidi, Kupambana na Misimamo Mikali n.k. Mbinu na sera hizi zimewagawanya Waislamu katika makundi ikiwemo wale wanaokubali kutenganisha Dini na maisha, misingi ya Uhuru inaozalisha ushoga, uzinifu, utumiaji

*Endelea Uk..3*



Email: uqab@hizb.or.ke

wa vileo nk, Uchaguzi wa kilaghai wa kiDemokrasia n.k kuwa ni 'Waislamu Poa" na Waislamu wanaopinga yote hayo kwa kujifunga na Uislamu wao ima kibinafsi au kama Jamii na kuulingania Uislamu kama Mfumo na kufanya mikakati ya Kusimamisha Serikali ya Kiislamu ya Khilafa kwa njia ya Utume ili isimamie hali za walimwengu na iendeshe mambo kwa mujibu wa Al-Qur'an, Sunnah, Ijmaa Sahaba na Qiyas basi wao huitwa "Waislamu Wenye Misimamo Mikali".

Hapa nchini Kenya baadhi ya Sheria, Mbinu au Sera ambazo Serikali imepitisha ni pamoja na:

1. Sheria ya Kukinga Ugaidi ya 2012 "Prevention of Terrorism Act 30 of 2012"
2. Sheria ya Usalam (Mabadiliko) ya 2014 "Security Laws (Amendment) Act, 2014"
3. Mikakati ya Kitaifa ya Kupambana na Misimamo Mikali "National Strategy to Counter Violent Extremism"
4. Balozi Maalumu ambaye pia ni Msimamizi wa Kituo cha Kupambana na Ugaidi na Misimamo Mikali - Kuhudhuria Kongamano la Kumi na Sita la Kimataifa lililoandaliwa na Taasisi ya Kimatiafa ya Kupambana na Ugaidi "International Institute for Counter-Terrorism (ICT) 16th International Conference" – 13 Septemba, 2016, Sharon Hotel, Herzliya 'Israel'

Kutokana sheria, mbinu au sera hizo kumetokea dhulma za kila aina dhidi ya Umma wa Kiislamu Ulimwenguni na hapa nchini Kenya. Hali ni ya kusikitisha mno tukiangalia yanaowafika Waislamu nchini Syria, Palestine, Afghanistan, Uzbekistan, Jordan, Iraq, Burma, Yaman n.k wote wanapitia hali ngumu ikiwa ni juu ya pazia iliyomakinishwa na kupigiwa debe ulimwenguni kote kama "Kampeni Dhidi ya Misimamo Mikali na Ugaidi" ilhali nchi zinazokubali kubebeshwa na kushiriki kikamilifu katika Kampeni hiyo hatari wakipewa mabilioni ya pesa ikiwemo Kenya ambayo hivi sasa ishapokea zaidi ya Bilioni Ksh.20 za kupambana na Ugaidi pamoja Misimamo Mikali! Madhila haya yanawakumba Waislamu lakini lakushangaza ni kuwa vyombo vya habari ambavyo jumla yao vinamilikiwa na mabwenyenye wanaokula njama na Serikali tawala pamoja na Nchi za kimagharibi kuhakikisha kuwa wanajenga mazingira munasaba ya kuhalalisha mauaji ya Waislamu na kuwapongeza na kuwasifu wasimamizi pamoja na taasisi husika za kupambana na ugaidi kwa kazi nzuri! Napia wanatumika kukuza maoni na uamsho kuwa sambamba na mapendekezo ya wadhamini wa vyombo vya habari na ndio maana kabla hata uchunguzi kufanywa utasikia vyombo vya habari vikikurupuka na kusema "Gaidi kalipua mahali fulani au tukio lakigaidi limetokea "ilmuradi muhusika ni Muislamu!

Ndugu zenu Hizb ut-Tahrir Kenya tunawaambia musikate tamaa kwa wanayotupangia Makuffar.

وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَاكِرِينَ

"Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango." [Surah Al-Anfal:30]

Hakika hadhi na heshima yetu iko katika Uislamu kama Mfumo na hakuna anayestahiki kutuelekeza kuhusu Uislamu wetu isipokuwa Mwenyezi Mungu;

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمْ الإِسْلاَمَ دِينًا

"Leo nimekukamilishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe ndiyo Dini." [Al-Ma'idah:3]

Enyi Waislamu:

Ni amri kwenu kutoka kwa Allah (swt) kujifunga na Uislamu kikamilifu na wala sio kuukumbatia Uislamu unaopigiwa debe na Wamagharibu kwa mtizamo wao wa Kikafiri wa Kati na Kati uliotokamana na itikadi ya kutenganisha Dini na Maisha. Uislamu unatokana na Allah (swt) na Ameuridhia juu yetu kinyume na Wamagharibi wanaouchukia na kuupiga vita kimaneno na kwa vitendo.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا ادْخُلُوا فِي السِّلْمِ كَافَّةً

"Enyi mlio amini! Ingieni katika Uislamu kwa ukamilifu" [Al-Baqara:208]

Tofauti zetu za kimakundi au madhehebu zisitupelekee kuingia katika njama tuliyopangiwa na Wamagharibi kuwa eti kuna Muislamu wa Misimamo Mikali na Muislamu Poa. Hii ni Sumu ambayo lau tutainywa basi bila shaka tutajikuta tunazozana na pia hata kupigana kati yetu ambalo ndio lengo Wamagharibi wanalolifanyia kazi usiku na mchana haswa ikizingatiwa nguvu ya Uislamu na Waislamu ni Umoja na Ushikamano wao.

Magaidi Wakuu katika Vita dhidi ya Misimamo Mikali na Ugaidi ni Marekani na 'Israeli' ambao ni wazi kuwa vita hivi wame walenga Waislamu na Uislamu hususan tukizingatia kuwa Makongamano makubwa yanaandaliwa na 'Israeli' na udhamini mkubwa wa kifedha na sera za kufaulisha maovu na njama hizo ni Muamerika.

Tunatoa nasaha kwa Waislamu na yoyote Yule anae penda haki kuwa tusizinyamazie hali hizi zinapotokea bali tuzikemee pasi na kujali watakao laumu. Na pia haitoshi kuwasubiri Viongozi wetu wa kisiasa au Mashekhe kutuzungumzia kwani twaona vipi walivyobwaga majukumu yao. Baada yakuwa hawana lakusema kutetea Umma na madhila, ambalo lenyewe ni uovu, wao hudandia kulaani washukiwa kabla ushahidi kupatikana. Na haya wanayafanya si kwa lengo lengine illa kutaka kujipendekeza kwa serikali ili wapate maslahi au kukhofia maslahi yao yasipokonywe. Haya yamejitokeza wazi katika matukio ya hivi karibuni ya kushikwa Waislamu ovyo wakiwemo wanawake na watoto na mara nyengine hata kupotezwa. Pia hatuna budi ili madhila haya yaondoke ni lazima tujitahidi kufanya ulinganizi wa kurudisha tena maisha ya Uislamu kupitia kusimamisha serikali ya Kiislamu ya Khilafa kwa njia ya Utume. Mauaji, Mateso katika jela za kitwaghut n.k zisiwe ni tishio kwetu bali tuziangalie kama mitihani itokayo kwa Allah s.w.t na iliyojaa kheri nyingi ikiwemo kupata pepo kwa wanaokuwa na subra ya hali ya juu. Na tusiwe na shaka na Dini yetu juu ya kurudi kwa Ngao yetu ya Khilafah


*Endelea Uk..4*

kwa Njia ya Utume:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ
وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِنْ
بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ
كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

"Mwenyezi Mungu amewahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema. Ya kwamba atawafanyiaa makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wa kabla yao, na atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao."
[Surah An-Nur 24:55]

**Hizb ut-Tahrir Kenya**
**Rajab, 1438**
**Aprili, 2017**



# Bajeti ndani ya Serikali za Kirasilimali Haitatui Mzigo wa Maisha ya Juu kwa Mtu wa Chini

**Habari:**
Alhamisi 30 Machi, 2017; Waziri wa Fedha Henry Rotich nchini Kenya alisoma hotuba ya bajeti ya mwaka 2017/2018 ambayo ni kunyume na mazoea ya hapo awali ambayo hotuba hiyo hutolewa kila mwezi Juni bungeni.
Huku Serikali ikifungua mifuka ya bajeti ya 2017/2018 miezi mitatu mapema, mtizamo wa Wakenya utakuwa ni kuangalia ni vipi trilioni Ksh.2.6 itabadilisha maisha yao. Henry Rotich alisema kuwa kauli mbiu ya bajeti hiyo ni "Kubuni Ajira, Kupeana Maisha Bora kwa Wakenya Wote"; bajeti hiyo itaifanya nchi kuwekeza katika vinavyokuza ajira hususan kwa vijana.

**Maoni:**
Bajeti ya 2017/2018 iliyosomwa Bungeni kama ilivyokuwa miaka mingine imemuacha mwananchi wa kawaida kushangaa na kutojua nini kinachopelekea kukua na kwa asilimia kubwa kwa bajeti hiyo kutokea trilioni Ksh.1.2 mwaka 2012/2013 hadi trilioni Ksh.2.2 mwaka 2017/2018 ambayo ni mara mbili zaidi ndani ya muda wa miaka mitano (5)! Huu ukiwa ni mwaka wa uchaguzi wabunge wanapigania bilioni Ksh.40.2 kama kiinua mgongo chao ambacho ni kinyume na pendekezo la Hazina ya Kitaifa iliyopendekeza bilioni Ksh.36. Kuna wasiwasi kuwa Wanachama wa Bunge la Kaunti nao wametoa shinikizo nao wapewe kiinua mgongo. Mishahara na marupurupu ya wanasiasa yamekuwa sehemu ya lawama kuwa inapelekea kutohimili kulipa mishahara ya nyanja tofauti tofauti ndani ya sekta ya umma. Madaktari, wauguzi, wahadhiri na walimu wamekuwa katika migomo na kusitisha utendajikazi wao kwa kushinikiza kuongezwa mishahara. Wanaoumia wakiwa ni Wakenya wa kawaida ambao wamekaa bila huduma kutoka kwa kikundi hicho hicho ambacho kina tia mfukoni takribani nusu ya ushuru wake. Hili linapelekea kuzidi kwa mzigo wa kulipa mishahara ambao hivi sasa unachukua takribani asilimia sabini na tano (75) ya bajeti.

Huku bei za vyakula zikiwa juu mno, uchumi wa nchi umesakamwa na deni la trilioni Ksh.3.8 na baadhi ya ahadi za uchaguzi hazijatimizwa; Wakenya walikuwa makini wakimsikiza Waziri wa Fedha Henry Rotich akielezea namna serikali ilivyoazimia kutumia ushuru wao tukielekea katika uchaguzi Agosti 8. Mamilioni ya Wakenya wanaojitahidi kukidhi mahitaji yao, kutafuta ajira na kuwasaidia familia zao hivi sasa wataingiza mkono mfukoni zaidi ili kulipa ushuru zaidi wa trilioni Ksh.1.7 mara mbili zaidi ya walivyolipa mwaka 2013 (bilioni Ksh.847). Hii ikiwa ni licha ya zaidi ya nusu ya ushuru huo utatumika kuwalipa Wakenya 700,000 ambao wanajumuisha chini ya asilimia mbili (2) ya idadi ya watu nchini! Malalamiko ya juu ni kuwa bajeti hii ya trilioni Ksh.1.7 inatazamiwa kukamuliwa kutoka kwa walipa ushuru ambao mapato yao hayaja ongezeka kwa miaka sasa, ongezeko la mfumuko wa bei na kupotea kwa mapato kutokana na kufutwa kazi au kutaifishwa na makampuni ili yaweze kupunguza gharama ya sehemu watakazoweza kuhimili katika bajeti zao ikiwemo kuwalipa wanaowafuta na bima zao. Pengo la bajeti ya 2017/2018 litazibwa kwa mikopo kama kawaida ambayo itapelekea deni la kitaifa kukuwa na kufikia trilioni Ksh.4 ambalo pia linatakiwa kulipwa na mtozwa ushuru! Yote haya na shida nyingi tunazoziona kama taifa na wanadamu si kwa sababu ya lolote lile bali ni kwa utungaji sheria zetu ambazo ni kinyume na za Muumba ambaye anajua na anaufahamu fika kuhusu huu ulimwengu zaidi kuliko sisi. Usomwaji wa bajeti hauna jipya isipokuwa ukhaini wa kisiasa unaolenga kuudanganya umma ambao unaataabika kwa maangavu yakiwemo njaa, magonjwa na kusambaratika kwa uchumi. Bajeti hii kama bajeti nyinginezo ndani ya serikali za kirasilimali huwa hazitatui mzigo wa hali ngumu ya maisha kwa mtu wa kawaida. Majanga ya kiuchumu yataendelea kuwakumba kwa kuwa serikali zimekumbatia ufisadi wa nidhamu ya kiuchumu ya kirasilimali. Hivyo basi tusitarajie mabadiliko yoyote ya kiuchumi kutokana na kusomwa kwa bajeti kwani maadamu Kenya imejifunga na umagharibi/urasilimali.

**Bakari Mohamed**
**Mwanachama wa Ofisi ya Habari ya Hizb ut-Tahrir Kenya**


Email: uqab@hizb.or.ke




# Raisi Mpya wa Somali Ametangaza kuwa Nchi yake ni "Eneo la Vita"

Raisi mpya wa Somalia aliyechaguliwa hivi majuzi Mohamed Abdullah "Farmajo" ametangaza kuwa Somalia kuwa ni Eneo la Vita. Tangazo hilo alilolitoa Alhamisi 5 Aprili, 2017 linakuja muda mfupi baada ya hali ya usalama kuzidi kudorora ambapo hivi majuzi bomu liliripotiwa mji mkuu wa Mogadishu na kuua watu saba. Akiwa amevalia magwanda ya kivita aliwataka wapiganaji wa Alshabab wasalimu amri. "Tunawaambia vijana wapiganaji wa Alshabab, waliochanganywa akili kuwa wana siku sitini (60) za makataa ili kuweka chini silaha zao wanazozitumia kuwaua watu wao na wasalimu amri waje kwetu" alitamka. (Aljazeera)

Mwanzoni mwa Machi, 2017 utawala wa Trump ulichora mpango mpana wa kijeshi ambao ulijumuisha kitengo maalumu cha kijeshi cha kupigana na makundi yaliyojihami ndani ya Somalia. Taasisi maalumu ya Pentagon tayari imetuma mapendekezo ikulu White House ili kuruhusu Kitengo Maalumu cha Kijeshi cha Marekani kuongeza msaada kwa Jeshi la Taifa la Somalia na kulipa Jeshi la Marekani nguvu zaidi ili kuweza kutupa mizinga angani.

Jeshi la Marekani kuingia vitani sio jambo jipya bali ni muendelezo wa mipango iliyowekwa na utawala wa Bush. 4 Disemba, 1992, Raisi wa Marekani George H.W.Bush aliwahutubia wa Marekani, kuwaambia kuwa wanajeshi wa Marekani watatumwa kwenda Somalia. 1993 Marekani ikatangaza kampeni ya kijeshi iliyoitwa Rudisha Matumaini "Restore Hope" ambayo ilijumuisha vikosi vya kimataifa na ambavyo vilijulikana kama Muungano Maalumu wa Kijeshi UNITAF au "United Task Force". Oparesheni hiyo ilibuniwa baada ya kuondoshwa mamlakani Siad Barre ambaye alikuwa kibaraka wa Marekani na ambaye utawala wake uliwatengea takribani thuluthi mbili za Somalia kwa makampuni ya Mafuta ya Kimarekani ikiwemo Conoco, Chevron na Philips.

Tangu wakati huo Marekani imekuwa ikimakinisha muelekeo wa kisiasa wa taifa hilo kwa kusimamisha viongozi vibaraka ambao wameletea Somalia maangamivu na kupinduliwa mara kwa mara. Kwa miaka sasa Marekani imekuwa ikiwapa wakuu wa makundi zana za kivita ambao kinaya ni kuwa wamekuwa ndani ya serikali zizo hizo. Mfano mzuri ukiwa ni mpango wa Marekani kuigawa Somalia ili iwe maoneo tofauti na kuyashajiisha maeno yaliyo na kawi nyingi kama Juba land kusitisha mizozo na kuwa chini ya maslahi yake. Kwa hiyo si ajabu kuona tamko hilo la Farmajo likitolewa muda mfupi baada ya mipango ya Marekani kuzidisha mashambulizi ya kijeshi Somalia.

Somalia nchi iliyojaa rasilimali asili nyingi imetangazwa na Marekani kama eneo "salama kwa magaidi" ili kupata sababu ya kuweza kuivamia na kufikia maslahi yake ya kichumi. Mafuta yaliyogunduliwa na tawala za Uingereza na Italia; kisha baadaye makampuni ya Ufaransa na Marekani yakaanza kuzozana na makampuni ya Uingereza na Italia ili kumiliki haki ya kibiashara na kufanya tafiti za mafuta. Hayo yote yamepelekea taifa la Somalia kuwa ndio kiwanja cha vita kati ya Ulaya na Marekani ili kupata haki ya kudhibiti utajiri wa mafuta ya Somalia. Ulaya ikiongozwa na Uingereza kuipiga Marekani kupitia kuwaunga mkono makundi ya kivita nchini humo na kuyatumia mataifa vibaraka ikiwemo Kenya, Djibout na Uganda. Marekani nayo ikiwaunga mkono wapiganaji kupitia nchi kama Ethiopia na Sudan. Hiyo ndio asili ya mzozo wa Somalia.

Somalia hivi sasa iko katika janga kubwa la kibinadamu linalosababishwa na muendelezo wa ukame na ukosefu wa chakula cha kutosha kwa miongo kadhaa mpaka sasa. Hivi sasa zaidi ya watu wapatao milioni tano (5) ya wasomali wanahitaji msaada wa dharura ili kuwalinda na ukosefu wa chakula. Huku serikali zilizofeli zikitoa ahadi tupu ikiwemo pamoja na utawala uliopo sasa, Somalia inaendelea kushuhudia maumivu ya mgawanyiko, vita vya kimbari na ukosefu wa chakula cha kutosha. Mashirika ya Kimataifa ya jiitayo mashirika ya Waislamu ikiwemo Muslimu World League, Organization of Islamic Countries pamoja na mashirika ya kimataifa mengine ima hayajaangazia kwa undani zaidi au hawajafanya chochote kuepuka hali hiyo!

Somalia kama ardhi yoyote ile ya Waislamu na nchi ya Kiafrika imejipata kwa muda mrefu ikitawaliwa na mataifa ya kikoloni. Tangu Uingereza ikidhibiti kaskazini-magharibi ya sehemu ya Somalia kwa zaidi ya miaka sabini (70), iliitwa British Somalia. Italia ilidhibiti kusini kwa zaidi ya miaka hamsini (50) na illitwa Italia Somalia na Ufaransa ilidhibiti hii inayoitwa leo Republic of Djibout. Pamoja na nchi jirani, kwa makubaliano na nchi koloni hususan Uingereza walimiliki eneo kubwa la sehemu hiyo. Hivyo basi, Ethiopia ambayo mwanzoni ilijulikana kama

Endelea Uk..6

Abyssinia iliteka eneo la Ogadin na Kenya nayo ikateka eneo kubwa la ardhi kusini.

Hali hii ya kutamausha itabadilika tu kwa kusimamisha Serikali ya Kiislamu ya Khilafah kwa Njia ya Utume. Kusimama kwake kutatua matatizo msingi yanayoikumba Somalia na ulimwengu mzima.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Kupambana na itikadi kali: Kampeni hatari ya kuwalazimisha Waislamu kujifunga na fikra za Kisekula



Serikali imeanzisha kitengo maalum cha kupambana na itikadi kali. Jopo hili linalojumuisha makatibu wakuu na ofisi ya inspekta mkuu wa polisi linalenga kutumia nguvu zake zote za kuweza kukinga na kupambana na misimamo mikali, ni moja wapo ya kampeni ya pamoja ya kitaifa inayodaiwa kufikia lengo la kupata usalama, maendeleo, na utangamano wa kitaifa. Msemaji wa serikali Erick Kiraithe alisema kuwa serikali imeanzisha kampeni hii ya kitaifa kwa lengo la kuilinda Demokrasia, utangamano na maendeleo dhidi ya hatari ya mawazo/ yatokamanayo na mafunzo ya itikadi kali, usajili wa vijana kwenye makundi na kukabiliana na mashambulizi.

Kwa haya, harakati ya Kiislamu ya Hizb ut-Tahrir/Kenya ingependa kutaja yafuatayo:-

Kitengo hiki kifanyacho kazi chini ya ule mkakati wa kitaifa wa kupambana na itikadi kali ulioanzishwa na Rais mwezi Septemba mwaka jana (2016), hakika ni sehemu tu ya kampeni kubwa inayoongozwa na Marekani ya kuushambulia Uislamu kifikra na kisiasa. Mfano wa karibu ni pale utawala wa Trump mwezi Februari mwaka huu ulipoweka wazi mpango maalumu unaojulikana kama ‘kupambana na itikadi kali’ ama Counter Violent Extremism (CVE), ‘Kupambana na itikadi kali za Kiislamu au ‘kupambana na misimamo mikali ya Kiislamu’. Trump alibainisha wazi kuwa kampeni zote hizi ni kupambana na Uislamu. Kwa kuwa Marekani inajizatiti katika kueneza nidhamu yake mpya ya kileberali (New World Order) kufuatia kuanguka kwa mfumo wa kikomunisti mwaka 1991, hivyo siajabu kwa nchi kama Kenya na ulimwengu wa tatu kiujumla kuchukua mpango huu muovu.

Kampeni hii inaelekezwa kwa lengo la kupinga Uislamu na kuzuia utekelezwaji wake sio tu kwa Waislamu nchini Kenya bali kwa ulimwengu kwa ujumla. Huu ni mpango wa kuendeleza kupachika mawazo na fikra za chuki katika mabongo ya Wasokuwa Waislamu dhidi ya Uislamu na wakati huo huo kuwaogopesha Waislamu wasishikamane na mafunzo ya matukufu ya Kiislamu yaliyoteremshiwa bwana Mtume Muhamad (saw), badala yake wachukue na kushikamana na fikra za kisekula.


Jambo muhimu twapenda kutaja hapa ni kuwa msamiati wa Siasa kali na mafunzo yenye itikadi kali yana beba maana pana ya kisiasa ambayo huweza kutumiwa kiholela hivyo kubuni nafasi itakayoruhusu serikali kutumia sera isojulikana kama vile utumiaji wa hatua za kimabavu dhidi ya Waislamu na kuwalazimisha kubadilisha itikadi na misimamo yao. Kwa kuwa kufeli kwa mfumo wa kibepari kuko wazi leo Ulimwengu mzima kiuchumi na kisiasa na kijamii, hivyo Marekani kwa sasa iko mbioni ikifanya juhudi kubwa ya kuzuia Mfumo mbadala nao ni Uislamu ulio na uwezo mkubwa wa kutatua matatizo ya kisiasa,kiuchumi na kijamii yanayokumba dunia leo. Hivyo ni jukumu la Waislamu kusimama na kupaza sauti zao kuulingania Uislamu kwa njia safi ya kifikra na Kisiasa tena isotumia mabavu ili kuonesha jinsi Uislamu ulivyokuwa ni mfumo kamili na muongozo kwa wanadamu wote.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari Hizb ut Tahrir in Kenya**



Email: uqab@hizb.or.ke

# Namna ya Kuhesabu Pato la Taifa (GDP) Katika Uchumi wa Kiraslimali




Licha ya kuinuka (kuimarika) kwa uchumi nchini Kenya kuanzia mwaka 2012, ukosefu wa ajira umeongezea kutoka aslimia 44 hadi 47 kwa mujibu wa utafiti uliofanywa Taasisi ya Fedha ya Kiulimwengu (IMF) Jedwali la juu linaonyesha ukuaji wa uchumi wa Kenya kutoka mwaka 2008 hadi 2015

Hifadhi za kenya ziliongezeka kutoka Dola 6.599 billioni mpaka Dola 70 kutoka mwaka wa 2013 mpaka 2015 na mfumko wa bei ukapungua kutoka asilimia 14 mwaka 2011 mpaka asilimia 6.2 mwaka wa 2015. Yote haya ni ishara ya uchumi bora na bei nafuu kwa wateja. Lakini licha ya yote hayo, maisha yanazidi kuwa magumu kwa raia wa kawaida.

Fomula inayotumika kuhesabu pato la taifa(GDP) kwa nchi ni kujumuisha matumizi ya kibinafsi, uwekezaji wa jumla, uwekezaji wa serikali, matumizi ya serikali.

Matumizi ya kibinafsi ni jumla ya bidhaa na huduma zinazotumiwa, na uwekezaji jumla ni idadi jumla ya viwanda vilivyopo na vilivyo asisiwa kwa mwaka flani. Uwekezaji wa serikali ni mapato yote ya nchi na matumizi yake ni yale matumizi ya kawaida mahsus kwa mwaka wa fedha.

Kwa kuwa hifadhi ya pesa inayotumika na banki kuu ya Kenya ni sarafu ya Dola, fomula inadhihirisha wazi kua thamani ya Dola kwa bidhaa na huduma nchini na zinazouzwa ng'ambo kwa mda maalum ndio huonyesha kukuwa kwa uzalishaji kutokana na viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo ambavyo humilikiwa na watu wachache kwenye jamii na haiathiri katika kukuza hali ya maisha ya raia wa kawaida mwenye kuonekana kama mteja na hutumika kama kipimo cha kuonyesha jinsi viwanda hukua kupitia mauzo yao.

Kwa kuhakikisha kuwa fomula inaonyesha kukua kwa uchumi ambao utaboresha hali ya maisha ya mwananchi wa kawaida, matumizi ya kibinafsi basi yasitumike kama kipimo cha bidhaa na huduma ngapi zilizotolewa na kuuzwa kwa bei gani na viwanda bali itumike kuhesabu uweza wa wananchi wa kawaida kumudu bidhaa na huduma zinazotolewa na viwanda kulingana na mapato yao.

Katika mfumo ambao matajiri 8 waliobadilisha raslimali za Ummah na kuzibinafsisha wakimiliki utajiri sawiya na watu masikini bilioni 3.6, fomula ya kuhesabu pato la taifa (GDP) huhesabu mapato yao tu kuwaezesha kutumia ushawishi wao kuathiri kutangaza fomula kama hizi kupitia mabunge na taasisi za elimu. Hao matajiri wachache hudhamini takriban taasisi zote za utafiti katika vyuo vikuu vikubwa duniani ambavyo hutengeza fomula kama hizi katika nchi zilizoendelea na kuziteremsha chini mpaka taasisi za elimu za nchi ziitazwo za ulimwengu wa tatu.

Serikali ya Khilafah iko na haki ya kusimamia rasllimali zote za Ummah kwa niaba ya wananchi wake. Hii itahakikisha rasllimali yoyote ya Ummah inayotumika na sekta ya viwanda au huduma ama bidhaa yoyote zinazozalishwa nazo mapato yake yatatumika moja kwa moja katika kuboresha hali ya maisha ya wananchi wake kama kujenga barabara, shule, hospitali, masoko na kadhalika.

Mpangilio wa Zakah pia utahakikisha kuwa asilimia 2.5% ya utajiri utatozwa kutoka kwa wale mali yao imefikisha kiwango maalumu kinachotakiwa kisheria kutozwa (Nisab) na kupelekewa mafukara, maskini, wapita njia, wakusanyaji zakah, waliojitolea kwa njia ya Allah, wenye nyoyo zao zilizosalimu kwa imani/haki /waliosilimu na wale walio katika utumwa na madeni. Hii ni kusawazisha mzunguko wa mali baina ya watu na hivyo basi kutengeza mazingira bora ya ufanisi amabyo fomula ya kuhesabu GDP itawiyana na kukuwa kwa uchumi na kuimarisha maisha ya raia ndani ya Khilafah.

**Bakari Mohamed Dziphengo**
**Mwanachama Katika Ofisi ya Habari ya Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Nani wa Kulaumiwa Kati ya Wazazi Na Mfumo?



Uislamu kama mfumo kamili wa maisha uliofaradhisha sheria kwa waislamu na wanadamu nazo ni wajibu kwa kila mwislamu kuzitekeleza. Miongoni mwa sheria hizi ni kukuza watoto wawe na mienendo ya kiislamu. Ni jukumu la kila mzazi kuhakikisha watoto wao wamekuzwa kwa misingi ya kiislamu, na hivyo ndivyo walivyokuzwa watoto wa wema waliotangulia. Na mtoto anakuzwa kiislamu kuanzia siku anapozaliwa kwa kuadhiniwa sikio la kulia na kukimiwa sikio la kushoto, na kufunzwa mengine akiwa na umri wa miaka saba.

Hukuzwa kutokana na malezi haya mabarobaro na mashababu wa kiislamu kama Ali ibn Abi Talib na wengineo waliosimama na Uislamu mpaka mwisho wa uhai wao. Walielewa jukumu lao mbele ya Uislamu baada ya kufahamishwa na kukuzwa kifikra za kiislamu jambo ambalo halifahamiki na mashababu wetu wa sasa. Vijana wamejishughulisha na anasa za kidunia wakasahau majukumu yao kama mabarobaro wa kiislamu.

Mbali na shughuli za kidunia zinazo washughulisha ndugu zetu, kuna waliojiingiza katika magenge ya wezi wakihangaisha umma, chumo lao likitoka kwa wanawake. Mamama wamekuwa hawana amani tena wakihangaishwa na waume nawatoto wao wenyewe. Ulimwengu umekuwa mgumu kwao kwani kila kona wanayopitia ni vurugu kutoka kwa vijana hao waliojitolea kufa kwa ajili ya tamaa ya kidunia. Lakusikitisha na kuhuzunisha ni kuwa vijana hawa ni wa kiislamu ambao ndio msingi wa kueneza da'awa ya kiislamu ambayo ni huruma kwa walimwengu wote. Wako wapi kina Ali bin Abi Talib?

Kuna maswali mengi yanayokula mtu akili; je? wazazi ndio waliozembea katika malezi yao au ni mazingira ndio yanayoharibu watoto na mabarobaro wa kiislamu? Nakwa nini iwe kwa waislamu ambao wameletewa uongozi wa sawa kutoka kwa Muumba? Kwanini mabarobaro wetu wajifie ovyo kama mbwa chini ya mikono ya polisi kwa kupigwa risasi kila leo? Wazazi hamusikii uchungu watoto wenu wakiuwawa?

Maswali hapo juu yako na jibu moja thabiti nalo ni umuhimu wa kufanya kazi kuregesha serikali ya Khilafah kupitia kwa mwenendo wa mtu. Serikali ya kiislamu itachukua jukumu la kueka muundo wa seera utakao hakikisha miongoni mwao elimu zinafunzwa kulingana na Uilamu ikilenga kukuza kizazi kitakacho skumwa na ucha mungu na watoto wenye lengo la kunali radhi za mola wao kwa kudhibiti kupima matendo yao kwa misingi ya halali na haramu. Kinyume na vile tunavyo shuhudia katika muundo wa elimu katika nidhamu ya uraslimali iliyoundwa kuzalisha wafanyikazi na watumwa wa makampuni ya kimataifa ya kibepari ambao maoni yao ni faida iliyo kitwa imara juu ya kanuni ya ulaji! Hadi wakati huo utulivu kwa jamii kamwe hautashuhudiwa kwa sababu sehemu yake muhimu imeachwa katika huruma ya mfumo fisidifu wa kibepari na nidhamu yake ya kuvunda ambayo milele huleta huzuni na kushuhulisha si vijana tu lakini jamii nzima kwa ujumla.

**Mgeni Juma Salim**



Email: uqab@hizb.or.ke



## SWALI / JAWABU

# Siasa ya Kivitendo ya Marekani Juu ya Urusi Na China

**Swali**

Ametangaza Rais wa Marekani Obama katika tarehe 29/12/2016 ambapo ni wiki tatu kabla ya kuondoka kwake (madarakani), mfulululizo wa adhabu kali dhidi ya Urusi zenye kujumuisha kufukuzwa kutoka Marekani kwa idadi kubwa ya wanadiplomasia wa Urusi "ambao ni 35" na kufungwa kwa balozi/ majumba ya wanadiplomasia wa Urusi huko Maryland na New York kwa kisingizio cha ujasusi… Hali yote hii tete inatokana na tuhuma za Marekani dhidi ya Urusi juu ya udukuzi wa kielektroniki katika uchaguzi wa Marekani…Je, jambo hili ndilo lililolazimisha hatua zote hizi? Au kuna sababu nyenginezo na hasa kwa kuwa Trump anatangaza kuboresha uhusiano na Urusi wakati ambapo Obama anauchafua! Wajazakallahu Khayraa.

**Jawabu**

Ili jawabu liwe wazi, na tuchunguze waqia iliyotokea kisha tuchunguze maswali yaliyoulizwa.

KWANZA: Ama waqia iliyotokea ni sahihi; kwamba uongozi wa Marekani uliopo hivi sasa unatekeleza kivitendo kuchafua mahusiano ya Marekani na Urusi, na Urusi imefahamu ujumbe huu, ikawa majibu yake ya haraka kupitia msemaji wa Kremlin, Peskov kwamba "Adhabu za Marekani zina mwelekeo wa uvunjifu na uadui na si zakutegemea." Na akaendelea "Uongozi wa Obama unavunja mahusiano ya Urusi na Marekani kwa kuyamaliza baada ya kuwa tayari yamefikia hatua ya chini. Na akatangaza kwamba "Moscow itarejesha majibu muwafaka dhidi ya hatua za Marekani…" (Russia Today na French Channel, 29/12/2016). Na katika kuchafua mahusiano hayo, hatua za Marekani zilikuwa kama ifuatavyo:

1. Rais wa Marekani Barak Obama amesema tarehe 15/12/2016 kwamba "Marekani italipiza dhidi ya udukuzi wa Urusi kuathiri uchaguzi wa Marekani. Na Obama akaeleza katika idhaa ya "NPR" "Naamini kwamba hapana shaka ikiwa serikali yoyote ya kigeni inajaribu kuathiri kiwango kizuri cha uchaguzi wetu, sisi tuna haja ya kuchukua hatua." Akaongeza: "Na sisi tutajibu katika wakati na pahala tunamomuchagua". Na akaendelea "Baadhi (ya hayo malipizo) yatakua wazi na dhahiri. Na baadhi si hivyo…" (French 24, 16/12/2016). Na haya ndio majibu ya Marekani yamedhihiri katika adhabu alizozitangaza Obama dhidi ya Urusi.

2. Rais wa Marekani Obama ameishambulia Urusi kwa dhihaka na akaieleza kwamba Urusi ni "Dola ndogo". Na akasema "Wao ni wadogo na madhaifu, uchumi wao hauzalishi kitu kinachohitajika na wengine, mapato yake (Urusi ya mauzo hayatokani na chochote) isipokuwa mafuta, gesi, na silaha, na wala haiendelei…" (Russia Today, 17/12/2016)

3. Wizara ya hazina ya Marekani imetangaza tarehe 20/12/2016 kuweka vikwazo vipya dhidi ya wafanyabiashara saba wa Kirusi na mashirika manane ikiwa ni hatua ya kupinga Urusi kuichukua Crimea na mapambano yanayoendelea huko Ukraine. Haya ni kwa mujibu wa maelezo ya Wakala wa Habari "Reuters"… Na vikwazo hivi vinawalenga watu saba miongoni mwao ni makada kadhaa wa "Benki ya Urusi" ambayo huchukuliwa kwamba ipo karibu zaidi na mamlaka za Urusi, vile vile mashirika manne ya ujenzi na usafirishaji yanayofanya kazi Crimea iliyochukuliwa na Moscow… Na ukaongeza uongozi wa Marekani kwamba hatua hizi "Zinathibitisha kupinga ukoloni wa Urusi kwa Crimea, na kupinga kutambua jaribio la kuichukua rasmi…" (Dot Misr, 20/12/2016)

4. Mchezo wa Kimarekani wa kurejea kwa barnamiji ya vita vya nyota/sayari kulipiza dhidi ya kuendelea kwa Urusi kukuza silaha zake za nyuklia. Na katika muktadha huu sheria za Marekani zimebadilishwa ili kuruhusu kuongoza nguvu za kijeshi katika anga (hapana budi hapa kuonyesha kwamba baraza la Congress la Marekani limeingiza marekebisho mawili muhimu katika kielelezo cha kanuni wakati wa hatua ya kuithibitisha. Moja kati ya hayo yanafuta Washington kutuma kwa kiwango maalum cha missile shield. Wakati ya pili yanapelekea kuanzishwa kwa kazi ya kusaniisha imara vijengwa vipya katika mfumo huu kwa matayarisho ya kuutuma

*Endelea Uk..10*

angani hapo mbeleni. Na gazeti la "Los Angeles Times" limemnukuu Trent Franks, mwanachama wa Baraza la Wawakilishi kutoka chama cha Republican, na ni mkubwa katika walioleta marekebisho haya mawili, kukubali kwake kwamba hayo (marekebisho mawili) yanategemea mpango wa "Ari ya Kinga ya Kimkakati" uliozinduliwa na Rais Ronald Reagan katika mwaka 1983 na unajulikana vile vile kwa jina la "Vita vya Nyota/Sayari"… (Tovuti ya Dar el-Ikhbar, 24/12/2016). Na kinacholengwa ni (kuongeza) hali tete na Urusi.

5. Baraza la Wawakilishi la Marekani jana Ijumaa, 02/12/2016 limeridhia muswada wa sheria kuipa Wizara ya ulinzi ya Marekani dola bilioni 3.4 katika mwaka 2017 ili "kuizuia Urusi" na walioukubali ni 390 katika Baraza la Wawakilishi, walioupinga ni 30 tu mswada huu wa sheria. Na waziri wa ulinzi wa Marekani Ashton Carter alikuwa ameshatangaza wakati wa kuwasilisha kwa Congress muswada wa bajeti ya ulinzi kwamba Marekani inaongeza nguvu maeneo yake katika Ulaya kwa ajili ya washirika wake ndani ya NATO ili kukabiliana na uadui wa Urusi…" (Sputnik Russian Agency, 03/12/2016)

6. Na zaidi ya hayo, Marekani imeishusha hadhi ya Urusi katika kutatua mzozo wa Syria ikaifanya kuwa uwili wa Kerry – Lavrov ambao Moscow inaufurahia sana, na inautizama kama ni ishara ya kurejea ukubwa wa Urusi (Pia) ikaubadilisha na kuwa uwili wa Urusi – Uturuki . Na Marekani ijapokuwa ina mawasiliano ya kuendelea na msaada wa kuendelea juu ya juhudi za Urusi – Uturuki nchini Syria kulinda ushawishi wa pande (husika) kwa ajili ya kadhia zake nchini Syria. Isipokuwa muktadha wa Urusi – Uturuki badala ya Urusi – Marekani huzingatiwa ni kuishusha hadhi Urusi kimataifa na kuiweka katika hadhi ya dola kama Uturuki. Na hili yawezekana kuliona katika duru ya mbinu ya Marekani dhidi ya Urusi.

7. Hali hii ya kuongezeka kwa hali tete kwa hakika imeitisha Urusi. Basi katika majibu yake dhidi ya adhabu za Marekani alizoweka Obama, rais was Urusi alisema "Hakika Moscow inahifadhi haki yake ya majibu dhidi ya adhabu mpya za Marekani dhidi yake lakini haitoelemea katika kiwango cha uongozi wa Marekani wa sasa na wala haitolenga wanadiplomasia…" Na akaongeza kwa kusema: "Hatutowapa matatizo wanadiplomasia wa Marekani, wala hatutomfukuza yeyote. Na wala hatutomzuia mtu yeyote wa familia yao na watoto wao kutumia sehemu za umma walizozizoea katika sherehe za mwaka mpya. Zaidi ya hayo tunawaalika watoto wa wanadiplomasia wa Kimarekani wanaotambulika nchini Urusi kuhudhuria sherehe za mwaka mpya miladiya Kremlin…" (Russia Today, 30/12/2016). Na Moscow kutotoa majibu ya maana ya kutarajiwa, ambayo ni majibu mfano wake, kuna maana mbili:

YA KWANZA: Khofu kubwa iliyonayo Moscow juu ya malengo na matokeo ya mzozo huu wake na Washington.

YA PILI: Moscow inapiga hisabu kukabidhiwa uongozi mpya wa Trump Washington ili kurejesha muundo wa mahusiano ya nchi mbili juu ya misingi ambayo Moscow itairidhia. Na kwa kutokana Urusi ilivyo dhaifu kimtazamo wa kisiasa, inadhani kuwa Rais ajae, Trump atakua tofauti na Obama aliyemtangualia katika kuitazama Urusi, wakiwa wameghafilika kwamba asasi kubwa za uongozi nchini Marekani zote humuongoza Rais yeyote yule na kutoka chama chochote kile ili kuendelea katika kutekeleza siasa ya nje ya nchi yake. Na kwamba tofauti baina ya Obama na Trump ikitokezea hukusudiwa kutekeleza siasa ya Marekani iliyopangwa.

PILI: Kuchunguza yaliyojitokeza katika swali lililoulizwa:

1- Hakika adhabu hizi nzito kutoka uongozi wa Obama dhidi ya Urusi zinakuja katika hali ya Marekani kuridhika na uthabiti wa dori (jukumu) ya Urusi katika kutekeleza jukumu la kimataifa nchini Syria na Urusi itatekeleza jukumu hili kwa sura timilifu. Marekani imekamilisha kuihusisha Urusi katika (mzozo wa) Syria kwa kiasi ambacho haiwezekani kwa Urusi kutoka katika dimbwi la Syria. Na Marekani ilipokinai hilo ikaishusha hadhi ya Urusi ili iwe Serikali ya Uturuki ni wakala mshirika wake katika (mzozo wa) Syria badala ya kuwa serikali ya Marekani yenyewe… Yote hayo, kuzorota kwa mahusiano Marekani na Urusi na kuzidi mbinu dhidi yake hakuhusiani na mas-ala ya Syria. Basi Urusi inatekeleza kwa ithibati maslahi ya Marekani nchini Syria , na hili katu halina shaka kwa Marekani, bali hakika siasa ya Urusi nchini Syria imekuwa mtego kwa wafuasi wa Marekani – Irani na makundi yake, serikali ya Syria na Uturuki na wapinzani wenye kuelemea kwake – na haiwezi kutafuta siasa yake peke yake, na haiwezi kujitoa na kuiwacha Syria kwa jambo lisilojulikana. Na kwa ajili hiyo basi, inaimarisha na kutanua kambi zake za kijeshi Latakia na Tartous…Na haiwezi pia kudhibiti hali ya vita kwa kukosa wanajeshi wa ardhini iliowatayarisha hasa nchini Syria. Yote haya yanamaanisha dori ya Urusi nchini Syria imekuwa thabiti, bali imefungwa na siasa ya Marekani na wafuasi wake, wadau katika mzozo wa Syria… Na kwasababu hii basi, uzorotefu huu si kwa sababu ya Urusi kujiweka mbali na dori iliyopangwa kwa ajili yake na Marekani katika Syria, kwa sababu haijajivua dori yake iliyopangiwa na Marekani.

2- Na haifai mtu kufikiri kwamba vikwazo vya Marekani vilivyotangazwa na Rais Obama ni malipizo ya hasira dhidi ya udukuzi wa kielektroniki ambao huenda umechangia kushindwa chama cha Democrat na mgombea wake wa urais, Hillary Clinton. Hii ni kwasababu ingelikuwa hivyo, basi utawala wa Obama ungeliharakisha jambo hili la vikwazo kabla ya Baraza la Uchaguzi (Electoral College) halijathibitisha kuchaguliwa Trump kuwa Rais rasmi wa Marekani tarehe 19/12/2016… Ama kuianzisha kadhia hii baada ya kufuzu Rais mteule na kuthibitishwa na asasi

*Endelea Uk..11*

za katiba kwao, hili hutia shaka sana uhalali wa uchaguzi huu na pia uhalali wa Rais ajae, na hili, muda wa kwamba hakuna idara yoyote ya Marekani iliyokubali kushiriki (katika jambo hili)… Na lau tutajaalia kujadili kwamba, kuna hali zilizozuia kuwekwa vikwazo kabla ya kuthibitisha matokeo, basi yanayopelekea fahamu ya kisiasa ya madola makubwa (huwa) kama hawakulazimika kutangaza matokeo baada ya kuthibitika matokeo ya ushindi wa Rais, yatazaa dharura nyengine na sio udukuzi ili kuepuka kutiliwa mashaka ushindi wa Rais ajae. Na kwa kua vikwazo vimewekwa baada ya kuthibitisha rasmi ushindi wa Rais kwa hoja ya Urusi kujiingiza katika uchaguzi kwahiyo hii huwa si sababu ya kweli.

3- Na huenda ikasemwa kwamba maendeleo ya Urusi ya silaha zake za nyuklia na makombora ya mashambulizi (offensive missile) ndio sababu ya mbinu ya Marekani hivi sasa ndio majibu dhidi ya kauli za Rais wa Urusi. (Na kasema Rais Putin kauli yake katika mkutano na uongozi wa wizara ya ulinzi katika mji mkuu Moscow: "Ni wajibu kuinua ufanisi wa nguvu za kistretejia za kinyuklia (nuclear strategic forces) uwe katika kiwango kipya cha aina yake, kitakachoruhusu kuikabili hatari yoyote ya kijeshi itakayoitishia Urusi…" (Anatolia website, 22/12/2016)..

Jambo hili likiwa na athari kiasi kidogo cha uchumi wa Urusi kinaifanya juhudi ya Moscow upande huu kuwa si ya dhati. Haya ni baada ya kufaulu Marekani na magharibi kijumla kuua nguzo kuu za viwanda vya Urusi baada ya kuvunjika kwa Umoja wa Kisovieti, Urusi ikawa nchi yenye kusafirisha nje mali ghafi ijapokuwa imebakiwa na kiasi kikubwa cha viwanda vyake vya kijeshi, yaani Urusi haina juhudi za kushindana na Marekani kimataifa bali inaihitaji Marekani kuikubali dori ya Urusi katika siasa za kimataifa, mahitaji ambayo Marekani inayakataa yote kijumla. Hata Urusi inavyoitumikia Marekani Syria haijatosha kwa Marekani kuitambua Urusi kuwa ni dola kubwa na kuishirikisha katika kadhia nyengine za kimataifa, yaani (kuwa) Urusi ambayo imerithi Umoja wa Kisovieti na ikarithi kurasa kutoka katika historia ya makubaliano ya Marekani – Sovieti, ilikua inataraji kwamba ushirikiano wake na Marekani katika Syria utapelekea makubaliano kamili na ikawa inaiomba Marekani kushirikiana katika uwanja wa kimataifa. Na haya ikiwa yanaonesha dalili (ya matumaini) yoyote, basi yaonesha kasoro ya mtazamo wa kisiasa wa Urusi. Marekani imezichanachana kurasa za makubaliano na Umoja wa Kisovieti tangu wakati ilipokua (Sovieti) kuwepo kwake kulikua na athari yenye kuhisika ulimwenguni, vipi hivi sasa (Marekani) ikubali jambo hilo na dola ndogo – Urusi, kama alivyoielezea Obama?! Na Urusi kwa udogo huu mpya haiwakilishi utisho hasa kwa Marekani kuingia katika mvutano huu. Na yote haya yanamaanisha kwamba kauli za Urusi juu ya maendeleo ya silaha za nyuklia sio sababu ya uhakika ya Obama kuzorotesha mahusiano na Urusi.

TATU: Hivi ndivyo ilivyo sio hali zilizotangulia kutajwa ni sababu za kweli za uzorotefu huu, bali ni jambo jengine na inawezekana kulifahamu kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

1- Inawezekana kwa mwanasiasa yeyote na kwa wepesi kabisa kufahamu mtanziko wa kimataifa wa kimsingi unaoikabili Marekani leo ni kuinuka kwa China na kuweza kujenga uchumi mkubwa ambao unaweza kihalisi kutishia uchumi wa Marekani ulio wa aina ya kipekee duniani. Na zaidi ya hayo ni matumizi ya kijeshi ya China yanayoshika kasi ambayo yanapita matumizi nchi kama Urusi, Uingereza na Ufaransa kwa pamoja. Pia programu zake nyingi za kijeshi za kisiri. Kwa hiyo China imekua ni jambo lenye kuwashughulisha wanasiasa wa Marekani. Na kauli zote za maofisa wa Marekani hivi karibuni zimeelekezwa upande huu. Waziri wa ulinzi wa Marekani Ashton Carter ameeleza kwamba China imeinua uwezekano wa kuzidisha nguvu za kijeshi, na akasema kuwa Marekani ipo katika kipindi cha mpito… (Washington– "DPA": Kasema waziri wa ulinzi wa Marekani Ashton Carter katika kongamano la ulinzi jimboni California "Baada ya miaka 14 ya kupambana na waasi na kupambana na ugaidi… sisi tupo katikati ya kipindi cha mpito kimkakati ili kujibu changamoto za kiusalama ambazo zitazingatia mustakbali wetu. Na akasema Carter "China kutengeneza ardhi kwa kufukia bahari katika bahari ya China ya kusini (south China sea) kumenyanyua uwezekano wa kuongeza nguvu za kijeshi na hatari kubwa kutokana na makadirio mabaya..." (Al-Quds Al-Arabi, 08/11/2015). Na Rais Obama ana amini kwamba mustakabali wa Marekani una amuliwa leo katika Asia. Kasema Rais Barack Obama wa Marekani kuwa kampeni yake ya kurejesha uwiano ya siasa ya nje ya Marekani ili ishughulike kwa kiasi kikubwa Asia sio "uzushi wa kupita" wa urais wake… (Vientiane, Reuters. Siku ya saba, 06/09/2016). Na kusisitiza kwake Asia maana yake ni kukabiliana na China.

2- Imetangulia huko nyuma Marekani, katika kipindi cha Muungano wa Kisovieti kwamba kulikuwa kuna ukaribu baina ya China na Muungano kwasababu ya umoja wa chama cha kikomunisti, na ilivyokuwa Marekani wakati ule infanya kazi kidhati kuushinda Muungano wa Kisoveti, ikauchukulia kidhati ukaribu wake na China. Na ikawa inakwenda mbio kutenganisha ukaribu huu (wa Muunngano wa Kisovieti na China) na kuwa ni hatua ya kidharura ili kudhofisha Muungano wa Kisovieti na kuushinda. Na mpango wa Kissinger ukadhihiri katika wakati wake wa kuharibu mahusiano baina ya China na Muungano wa Kisovieti na alifaulu kiasi kikubwa kwa hilo… Lakini sasa hali halisi imebadilika, Marekani inahofu nguvu za China na inaona ukaribifu wake na Urusi kwahiyo inataka kuutenganisha ukaribu huu kama hatua ya kidharura ili kuiweka mbali China na kuidhoofisha, kama ilivyofanya hapo nyuma ila sasa ni kwa njia tofauti na haya ndio yaliyobainishwa na gazeti la

Endelea Uk..12

Washington Post. Likayanukuu haya Russia Today 18/12/2016 ifuatavyo: (Na iliandikwa katika makala kuwa kabla ya mwaka 45 Rais wa Marekani Nixon alijaribu kubadilisha muundo wa "pembe tatu" Muungano wa Sovieti – Marekani – China kwa kuweka rehani kuharibu maendeleo ya mahusiano na Beijing. Na katika tarehe 04/02/1972 Nixon akafanya mkutano na mshauri wake wa mambo ya usalama wa taifa wa wakati huo, Kissinger, ili kujadili ziara yake "Nixon" ijayo kuelekea China. Kissinger akasema kumwambia Rais Nixon katika mkutano huu kwamba "Wachina ni hatari sawa sawa kama Warusi na kihistoria ni hatari zaidi kuliko Warusi" Akamwambia zaidi Rais Nixon kwamba baada ya miaka 20 "Rais wa Marekani ajae akiwa mwenye hekima kama ninyi, atategemea Urusi katika siasa yake dhidi ya Wachina"

3- Kwa haya, inawezekana kufahamu vikwazo vya karibuni vya Marekani dhidi ya Urusi, pia shinikizo la Marekani dhidi ya Urusi linaloendelea kwa kitambo sasa. Na shinikizo hili ndilo walilonalo wanachama wengi wa Republican ndani ya Congress, yaani Rais ajae karibuni, Trump. Na zaidi pia chama cha Democrat. Shinikizo hili ndio siasa mpya dhidi ya Urusi kwa lengo la kuivuta iungane pamoja na Marekani dhidi ya China, kama kwamba Marekani inatamka , na pia ndio matamshi ya Urusi wazi wazi, ya kuwa uongozi wa Obama umevunja mahusiano ya Marekani – Urusi na kuyafikisha kuwa duni. Lakini Urusi ina fursa ya dhahabu kwa kuja Rais Trump ili kuboresha mahusiano yake na Washington! Yaani taasisi thabiti za utawala nchini Marekani kwa makusudi zinatumia muda uliobakia wa uongozi wa Obama kuharakisha hali ya mvutano na Urusi ili Urusi isiwe na njia ya uokovu na matarajio isipokuwa kwa maelewano na uongozi ujao wa Trump, uongozi ambao una amini maelewano ya kimaslahi (deal). Kwamba kuboresha mahusiano na Urusi hakupatikani ila baada ya maelewano ya kimaslahi makubwa pamoja nayo kuhusu China yenye faida. Ili kufikia jambo hili ni kwa kutumia udaku wa Rais ajae Trump wa kumheshimu Rais Putin. Na wawili hao yawezekana kuwa na itifaki kama marafiki dhidi ya China.

4- Kinachotilia nguvu hilo ni kuwa Rais ajae Trump tayari ameshazidisha uzorotefu wa mahusiano ya Marekani na China hata kabla hajashika wadhifa wake. Na anatangaza kuwa atatekeleza ahadi zake za uchaguzi kwa kuziwekea kodi kubwa bidhaa za China na kuzishajiisha kampuni za Marekani kurudi. Na hichi ni kitisho kikubwa cha kibiashara kwa China. Na akafanya haraka kufanya mawasiliano na Rais wa Taiwan katika jambo hatari kutangulizwa linaloashiria kwamba Marekani inazipekua nyaraka zake ili kuishinikiza China ikiwemo kitisho kwa Marekani kuachana na siasa "China moja" na kitisho hichi cha kisiasa ni kikubwa kwa China. Kwahiyo basi, la kwanza kati ya vipaumbele vya uongozi mpya wa Marekani ni kutibu kuinuka kwa China. Russia Today limenukuu tarehe 18/12/2016 kutoka Washington Post (Njia ya Rais mteule wa Marekani Donald Trump anasema kuwa yeye anaudurusu uwezekano wa kuangalia upya siasa ya Marekani kuelekea China. Na Trump akatoa wito wa kuanzisha sera kali kuelekea Beijing kwa njia ya kauli zake na maneno yake ya simu. Na Rais mteule wa Marekani alikua ameshafanya mawasiliano ya simu na Rais wa Taiwan na ndio mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka kadhaa. Na baadae Trump akaeleza katika mahojiano na chombo cha habari cha "Fox News" cha Marekani wasiwasi wake kuhusu usahihi wa Marekani kushikamana na misingi ya siasa ya "China Moja" ambayo Marekani imeiandaa tangu ziara ya kihistoria ya Rais Nixon kuelekea nchini China, katika jambo lililopelekea Trump kuituhumu China kufanya ujanja wa kibiashara).

5- Ama vipi yatakuwa maelewano ya kimaslahi ya Trump na Urusi dhidi ya China. Hakika Marekani haipangi kwa ajili ya uchumi wa Urusi ulio dhaifu katika kukabiliana na China. Wala vilevile haiweki mipango ya kutumia thakafa ya Urusi dhidi ya China. Urusi ni nchi ambayo haina thakafa yake hasa, baada ya kuporomoka ujamaa. Na jicho la Marekani liko wazi juu ya uwezo wa kijeshi wa Urusi ambao inawezekana kwa Marekani kuuwekeza juu ya China. Mfano kuilazimisha Urusi kushirikiana dhidi ya silaha za nyuklia za Korea ya kaskazini au kushirikiana juu ya kuitishia China katika usambazaji wa nishati kutoka Urusi au kutoka Asia ya kati, au hata kushirikiana kulazimisha siasa maalumu ya uhuru wa mambo ya usafiri wa bahari katika bahari ya China. Na kushiriki Marekani kwa bidii ili kuitoa China katika visiwa… Khiyari zote hizo, bila ya kutaja pia (amabalo linawezekana) kuisukuma Urusi kukabiliana na China moja kwa moja. Yote haya kwa Urusi ni kujiua yenyewe kimataifa. Lakini (ubaya wa mambo) Urusi yaweza kujikuta yenyewe imejiingiza katika siasa hizo za Marekani ili kujikweza nafsi yake eti kuwa dola kubwa!! Na katika jambo gumu kutafakari kwa Urusi ni kuweza kuzikimbia shinikizo za Marekani na kuziweka pembeni katika kuikabili China. Urusi ni mgonjwa kwa kuwa na kasoro ya mtazamo wa kisiasa, na maradhi yake haya yamekua sugu kwahiyo haiwezi kukadiria matokeo, kama inavyodhihirisha kuwa haijali kuwa Waislamu watafanya nini kwasababu ya kujiingiza kinyama Syria. Nayo ni kwasababu ya kasoro ya muono (wa kisiasa), inawaona Waislamu kwa wafalme na marais waliopo. Haioni kwao chochote kinachoitisha. Na wala haifahamu kuwa Marekani imejizuia yenyewe kutekeleza majukumu haya Syria kwasababu inajua kilicho mbali kwa hawa marais na wafalme. Kwa hivyo, vikwazo vya Obama na mvutano huu wa makusudi ni kwa lengo la kuiweka Urusi kipembeni na kuiburuza kwa Trump "rafiki yake" na njia kuwa safi kwa makubaliano ya kimaslahi ya Trump na Urusi ili kuitenga na China, bali ni kufanya uadui dhidi ya China! Hii ndio sababu yenye nguvu ya mvutano huo ambao Obama anaukusudia katika mwisho wa utawala wake ili kumuandalia njia Trump kulifikia lengo la kisiasa

*Endelea Uk..13*

la Marekani lililotajwa ambalo limewekwa na asasi za Marekani kwa ajili ya zama mpya kama inavyooneshwa na viashiria… Basi siasa ya Marekani huamuliwa na asasi na kutekelezwa na marais, (haijalishi) chochote kiwacho chama cha Rais.

6- Ama China inaelewa hatari inayoinyemelea kwa hiyo inaihadaa Urusi kwa vitega uchumi ijapokua kwa hadhari na inafanya mazoezi ya kijeshi kwa kushirikiana nayo. Na pia inapiga kura pamoja ya turufu pamoja nayo katika baraza la usalama hasa kuhusu Syria. Yote hayo kwa lengo la kuizuia Washington kuitumia dhidi yake. Lakini mtizamo wa uadui wa Urusi walionao wanasiasa wa Kichina umekita. Isipokua lugha ya maslahi mapya yanayolazimishwa na uchumi mkubwa wa China, na shida yake ya mali ghafi na raslimali ya nishati, ambavyo vyote hivyo vimejaa Urusi, hupelekea mtizamo huo wa uadui kuuficha nyuma ya pazia. Pia China inafahamu uadui wa Marekani upande wake, na si jambo la mbali kuwa yaliyotokea kwa Obama wakati wa ziara yake ya mwisho nchini China kuidhalilisha (China) ni miongoni yanayoashiria hayo (Katika ziara yake ya mwisho nchini China kama Rais wa Marekani alijikuta binafsi Rais Barack Obama akilazimika kutumia ngazi ya dharura sehemu  ya mwisho ya ndege iliyomchukua kuelekea uwanja wa ndege wa Guangzhou kuhudhuria mkutano wa kilele wa G20. Hayo si kwasababu ya (dharura ya) moto au tatizo la kiufundi, bali mamlaka za China hazikumpatia ngazi maalumu kwa ajili yake ya kushuka upande wa mbele wa ndege kama ilivyo kawaida. Wachunguzi wanaona kwamba China imefanya makusudi kitendo hicho kumdhalilisha Rais wa Marekani na hilo laonyesha ukubwa wa mvutano wa mahusiano baina ya nchi mbili (hizi) zinazotofautiana katika faili na kadhia kadhaa. Tangu mwanzo wake kutangaza Marekani na Korea ya Kusini kutuma makombora ya kinga (missile shield) kwenye ardhi ya Korea ya Kusini. Vilevile msimamo wa Marekani kuhusu mzozo uliopo baina ya China na Ufilipino katika bahari ya kusini ya China, na maamuzi ya karibuni ya Marekani kulazimisha ada ya ziada juu ya malighafi ya chuma cha pua cha China…) (Aljazeerah, 05/09/2016).

7- Na katika mikinzano ya wakati, mshauri wa usalama wa taifa na waziri wa mambo ya nje wa Marekani alietangulia, Kissinger, yeye leo mwenyewe ijapokua umri wake mkubwa ni bingwa wa upatanishi wa Urusi na Rais matarajiwa Trump. Na mwenyewe hufanya ziara Moscow na mikutano na Putin ili kumuelekeza upande huu, yaani upande wa ushirika na Urusi dhidi ya China. Na Urusi inalishabikia hilo ikidhania kwamba Kissinger anayapa umuhimu maslahi yake! (Amesema Dmitry Peskov, msemaji kwa vyombo vya habari wa Rais wa Urusi, kwamba Moscow inakaribisha ushiriki wa waziri wa mambo ya nje wa Marekani wa zamani, Henry Kissingerkatika kurejesha mahusiano baina ya Urusi na Marekani. Na Peskov akasema katika taarifa yake kwa vyombo vya habari leo Jumane kwamba Kisssinger, waziri wa zamani wa mambo ya nje wa Marekani ni mmoja kati ya wanasiasa wenye hekima nyingi, akili, na umahiri, na ana umahiri mkubwa katika mambo ya Urusi na katika kiwango cha mahusiano ya Marekani – Urusi…) (Arab Media Website, 27/12/2016) Na mwelekeo huu ndio vilevile unaooneshwa na baadhi ya vyanzo vinavyofuatilia mambo Ulaya. Russia Today tarehe 28/12/2016 limenukuu yafuatayo: (Gazeti la "Bild" la Ujerumani limeandika kwamba Kissinger anaamini kuboresha mahusiano na Urusi ni jambo la dharura akiangalia kuongezeka kwa nguvu za China. Na kwa kuwa waziri wa mambo ya nje wa Marekani ni mpatanishi mwenye ujuzi na kwa kuwa yeye mwenyewe binafsi amekutana na Rais Putin, basi karibu atakuwa mpatanishi wa kuyarejesha katika hali ya kawaida mahusiano baina ya nchi mbili. Na gazeti hili la Ujerumani linasema kuwa Trump anafanya bidii kuondoa vikwazo dhidi ya Urusi "kwa kuzingatia nasaha za Henry Kissinger" na una ashiria hayo vilevile "uchambuzi uliofanywa kutokana na ombi la vyombo maalumu vya Ulaya", unaotegemea taarifa ambazo zimepatikana kutoka katika timu ya mpito ya Rais Trump…) Yote haya yanaonesha kuwa Marekani inatekeleza siasa (yake) kivitendo dhidi ya pande mbili, Urusi na China, nguzo yake ya msingi ni kuisukuma Urusi kuitumikia katika medani ya China. Na uongozi wa Obama umeshaanza kwa kutilia mkazo hatua ya shinikizo dhidi ya Urusi, unapanga ili Rais ajae, Trump, awe ndie atakae ingia makubaliano ya kimaslahi (na Urusi). Wala Marekani haidhihirishi shaka yoyote juu ya ulazima wa Urusi kukubali shinikizo la Marekani na kuchangamka pamoja nayo dhidi ya China.

NNE: Namna hii ndio dola kubwa zinavyopambana na hata zisizokua kubwa pia katika kufanikisha maslahi yake, ijapokua kuna tofauti katika hili kulingana na tofauti za ushawishi baina ya dola hizo. Na asili wanayoshirikiana ni uovu na shari unaoonekanwa wazi (leo) ulimwenguni…

Na liumizalo ni kuwa Uislamu hauna serikali iliyoshika hatamu za mambo na kuurejesha Ulimwengu huu katika hali yake ya sawa na kueneza kheri kwenye pembe zake zote, si tu katika miji ya Uislamu bali pia pembezoni mwa miji ya Uislamu. Pamoja na hayo, Uislamu una wanaume

صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُمْ مَنْ قَضَى نَحْبَهُ
وَمِنْهُمْ مَنْ يَنْتَظِرُ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا

(waliosadikisha yale waliyomuahidi Allah, wapo ambao uhai wao umekwisha na wapo wanaosubiri, wala hawakubadili kabisa – ahadi yao) [Ahzaab: 23]

Na watairejesha Serikali ya Kiislamu kwa idhini ya Allah, Khilafah Rashidah ambayo itabadili uwiano katika dunia kuupeleka kwenye kheri,

إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْرًا

(Hakika Allah ni mwenye kutimiza tu jambo lake, na hakika amejaalia Allah kila kitu kiwango maalum) [At-Talaq:3]

**7 Rabiu thani,1438H**
**05/01/2017**